



CHAMA CHA WAFANYAKAZI WA TAASISI ZA ELIMU YA JUU TANZANIA

S.L.P 35928 DAR ES SALAAM, TANZANIA

Simu: +255 22 2401581, Nukushi: +255 22 2401582

Tovuti: www.thtu.or.tz Barua Pepe: thtuhq@thtu.or.tz

KUMB. NA. THTU/HQ/AD.01/0401.2026

04 Mei, 2026

TANGAZO LA NAFASI YA AJIRA

NAFASI: KATIBU MKUU WA CHAMA (Nafasi 1)

“Nia na Mwelekeo wetu daima ni kujenga, Taifa kwanza”



1.0 UTANGULIZI:

Chama cha Wafanyakazi wa Taasisi za Elimu ya Juu Tanzania (THTU) kinakaribisha maombi ya kazi kutoka kwa Watanzania wenye sifa na uwezo wa kujaza nafasi moja (1) ya Katibu Mkuu wa Chama kama ilivyoainishwa katika tangazo hili;



1.1 MAJUKUMU YA KAZI

- Kuwa Afisa Mtendaji Mkuu wa Chama na msimamizi wa shughuli za kila siku za utendaji wa THTU;
- Kusimamia utekelezaji wa maagizo na maazimio ya Kamati Kuu, Baraza Kuu na Mkutano Mkuu kwa mujibu wa Katiba, Kanuni na maelekezo ya vyombo vya Chama;
- Kuratibu maandalizi ya vikao vya vyombo vikuu vya Chama, taarifa za utendaji na kumbukumbu za sekretarieti;
- Kusimamia watumishi, rasilimali, mipango ya kazi na mifumo ya utawala ya Chama kwa kuzingatia taratibu zilizopo;
- Kuwa kiungo kikuu cha utendaji kati ya Chama, wanachama, waajiri, Serikali, wadau wa mahusiano kazini na taasisi nyingine kwa mujibu wa maelekezo ya vyombo vya Chama;
- Kutoa ushauri wa kitaalamu kwa vyombo vya Chama kuhusu uendeshaji, masuala ya kazi, majadiliano utatuzi wa migogoro na maslahi ya wanachama; na
- Kufanya kazi nyingine zinazohusiana na nafasi hii atakazopangiwa na vyombo halali vya Chama.



1.2 SIFA ZA MWOMBAJI

- Awe na Shahada ya Uzamili au Stashahada ya Uzamili katika Sheria, Usuluhishi na Uamuzi, Mahusiano Kazini, Taaluma za Maendeleo, Menejimenti ya Rasilimali Watu au sifa linganifu kutoka katika chuo kinachotambuliwa na Serikali; AU
- Awe na Shahada ya Kwanza katika fani husika kutoka katika chuo kinachotambuliwa na Serikali pamoja na uzoefu wa ngazi ya menejimenti ndani ya vyama vya wafanyakazi usiopungua miaka mitano (5);
- Awe na ujuzi wa kutumia kompyuta na mifumo ya ofisi;
- Awe na uwezo mzuri wa mawasiliano kwa maandishi na kwa kuzungumza; na
- Awe na uadilifu, tabia njema, uwezo wa uongozi, usiri na weledi katika masuala ya mahusiano kazini na utawala wa taasisi.



1.3 MUDA WA MKATABA

Kwa mujibu wa Katiba ya THTU, Ibara ya 105.1, ajira ya Katibu Mkuu ni ya mkataba wa muda maalum wa miaka mitano (5), unaoweza kuongezwa kulingana na utendaji na mahitaji ya Chama.



1.4 NGAZI YA MSHAHARA

THTU F21.



2.0 MASHARTI YA JUMLA

- Waombaji wote lazima wawe raia wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na wasiozidi umri wa miaka 55
- Maombi yote yaambatane na barua ya maombi iliyoandikwa kwa Mwenyekiti wa THTU Taifa, wasifu binafsi (CV) wenye majina na anuani za wadhamini wasiopungua wawili, nakala za vyeti vya elimu na taaluma, cheti cha kuzaliwa pamoja na vielelezo vya uzoefu wa kazi au ajira.
- Nakala za vyeti vinavyowasilishwa ziwe zimethibitishwa na Kamishna wa Viapo au mamlaka nyingine inayotambulika kisheria.
- Uthibitisho wa uzoefu wa kazi/ajira (barua, mikataba au vielelezo vinavyotambulika).
- Waombaji waliosoma nje ya Tanzania wahakikishe vyeti vyao vimehakikiwa na kuidhinishwa na mamlaka husika.
- Uwasilishaji wa taarifa au nyaraka za kughushi utasababisha mwombaji kuondolewa kwenye mchakato na hatua nyingine za kisheria kuchukuliwa.
- Waombaji watakaokidhi vigezo vya awali ndio watakaoitwa kwa ajili ya usaili.
- THTU ni mwajiri wa fursa sawa; wanawake na wanaume wenye sifa wanahimizwa kuomba.



3.0 ANUANI YA KUTUMA MAOMBI

- Barua ya Maombi ya kazi iliyosainiwa ielekezwe kwa Mwenyekiti, THTU Taifa
S. L. P. 35928
DAR ES SALAAM, TANZANIA
- Maombi yote yatumwe kupitia barua pepe: recruitment@thtu.or.tz
- Maombi yatakayowasilishwa nje ya utaratibu ulioainishwa katika Tangazo hili hayatafikiriwa.



Mwisho wa kutuma maombi ni tarehe **18 Mei, 2026** saa 6:00 usiku.

Limetolewa na: Mwenyekiti, THTU Taifa